Jarida la Wizara ya Afya

# Afya Habari

JARIDA LA MTANDAONI LA WIZARA YA AFYA | TOLEO, NO. 19, MEI 2024

TUNABORESHA AFYA
MTU NI AFYA • AFYA NI MTAJI




# TUNABORESHA AFYA

MTU NI AFYA, JALI AFYA YAKO




## BODI YA UHARIRI

**MWENYEKITI**
Dkt. John Jingu
KATIBU MKUU

**MHARIRI**
Englibert Kayombo

**MHARIRI MSAIDIZI**
Emmanuel Malegi

**WAJUMBE**
Englibert Kayombo
Emmanuel Malegi
Majid Abdulkarim
Said Nyaoza
Hassan Kimweri
Shaban Juma
Cletus Sanga
Abdulwaheed Madenge
Aisha Swahibu
Atley Kuni

**WASANIFU**
Englibert Kayombo
Said Nyaoza

@wizara_Afyatz
www.moh.go.tz

# YALIYOMO

Makamu wa rais dkt. Mpango aagiza wizara ya afya, TAMISEMI kuziwezesha idara za afya ....Uk 2





Barabara ya daraja la tanzanite kufungwa kila jumamosi asubuhi kupisha mazoezi .... UK 3

Waziri mkuu majaliwa aongoza watanzania kwenye mazoezi, Kulinda afya..... Uk 4





Serikali yatoa kipaumbele tafiti za kisayansi Naibu Waziri Mkuu Dkt. Biteko.... Uk 5

Serikali kuendelea kuboresha huduma za saratani Nchini - Dkt. Biteko.... Uk 6





Madaktari 1,109 kunufaika na ufadhili wa Rais Samia masomo ya ubingwa bobezi 2023/24.... Uk 6

Madaktari bingwa wa Rais Samia watasaidia kupunguza vifo vya watoto wachanga...... Uk 7



Tutazidi kuimarisha huduma za Ukunga kukabilina na vifo vitokanavyo na Uzazi .... Uk 8





Tanzania yapendekeza kunzishwa kwa vituo viwili vya umahiri kwa nchi za Afrika Mashariki .... Uk 9

Trilion 1.3 kutekeleza vipaumbele 10 vya wizara ya Afya.... Uk 10





Robot kutumika katika upasuaji wa Ubongo na Mishipa ya fahamu.... Uk 11

Asilimia 92 ya Wasichana wenye umri wa miaka 14 Wamepata chanjo ya HPV...... Uk 12





Dkt. Mollel aonya vikali maafisa utumishi kuingilia Majukumu ya makatibu wa afya .... Uk 13

Wataalamu wa vinasaba tumieni teknolojia kwenye Majukumu yenu: Dkt. Jingu.... 14





Wazazi tengeni bajeti ya ya kuwanunulia taulo za kike watoto wenu wa kike.... Uk 15



Wagonjwa wapya wa saratani 40 elfu hugundulika Kila mwaka, vifo 27 elfu . .... Uk 16

Wauguzi msingi wa huduma bora za Afya: Dkt. Mollel.... Uk 17





Hospitali zatakiwa kuimarisha karakana za vifaa tiba ili kusaidia katika utoaji wa huduma za uhakika..... Uk 18

Waganga wafawidhi, Madaktari Bingwa watakiwa kuendelea kuviishi viapo vyao..... Uk 19





Tanzania yaweka bayana ubunifu unaofanyika kufikia Afya kwa wote .... Uk 20

Aliyeteseka kwa miaka 10 na mawe kwenye kibofu afanyiwa upasuaji..... Uk 21





Madaktari Bingwa wa Samia wamrejeshea furaha Mtoto Jackline Singida.... Uk 22

# VIPAUMBELE VYA BAJETI YA WIZARA YA AFYA KWA MWAKA WA FEDHA 2024/25

1. Kuimarisha huduma za kinga dhidi ya magonjwa
2. Kuimarika upatikanaji na ubora wa huduma za afya ngazi ya Zahanati hadi Taifa
3. Kuimarisha mifumo ya ugharamiaji wa huduma za afya nchini
4. Kuimarisha huduma za afya ya uzazi, mama na mtotona watoto wachanga;
5. Kuimarisha upatikanaji na uendelezaji wa wataalam katika sekta ya Afya
6. Kuimarisha huduma za matibabu ya ubingwa na ubingwa bobezi
7. Kuendeleza na kusimamia afua za Tiba Asili na Tiba Mbadala
8. Kuimarisha upatikanaji wa huduma za magonjwa ya kuambukiza, yasiyoambukiza na mlipuko
9. Kuimarisha huduma za afya ya akili, utengamao na ulemavu
10. Kusimamia Tafiti na matumizi ya matokeo ya tafiti za afya



# MAKAMU WA RAIS DKT. MPANGO AAGIZA WIZARA YA AFYA, TAMISEMI KUZIWEZESHA IDARA ZA AFYA

**Na. Emmanuel Malegi**
**Kibaha, Pwani**

Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Dkt. Phillip Mpango ameziagiza Wizara ya Afya na Ofisi ya Rais-TAMISEMI kuziwezesha idara za Afya kuanzia ngazi ya Halmashauri za Manispaa, Miji na Majiji ili ziweze kuimarisha mifumo ya kutambua, kudhibiti na kukabiliana na magonjwa ya milipuko.

Dkt. Mpango amesema hayo Mei 9, 2024 Kibaha mkoani Pwani wakati akizindua Kampeni ya Mtu ni Afya inayolenga kutoa huduma za kinga ikiwemo usafi wa mazingira badala ya kuwekeza nguvu kubwa kwenye tiba.

Dkt. Mpango amesema ikiwa idara hizo zitawezeshwa zitaweza kujengewa uwezo wa kukabiliana na magonjwa ya mlipuko kwa kuimarisha mifumo ya kutambua, kudhibiti na kukabiliana na magonjwa.

"Endapo idara hizi zitawezeshwa licha ya kubaini na kukabiliana na milipuko pia zitaweza kufanya tafiti kuhusu magonjwa na kubaini jinsi yanavyosambaa, viashiria na vihatarishi lakini pia kujua tiba yake". Amesema Dkt. Mpango.

Aidha, ametoa rai kwa Halmashauri zote kuwatumia wahudumu wa ngazi ya jamii ambao watawezesha kufikiwa sehemu kubwa ya jamii na kuchochea mabadiliko ya tabia za wananchi na kuhakikisha usawa na urahisi wa utoaji wa huduma.

Kwa upande wake Waziri wa Afya Mhe. Ummy Mwalimu amesema Serikali ya awamu ya sita, chini ya Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan, kupitia Wizara ya Afya imekuwa ikiboresha huduma za afya kwa watanzania kwa kutilia mkazo masuala ya huduma za Afya kinga ili kudhibiti na kuzuia magonjwa ya kuambukiza na yasiyoambukiza yanayoweza kutokea kwenye jamii.

"Niwakumbushe kuwa, Kampeni ya Usafi wa Mazingira awamu ya kwanza (2012-2015) ilizinduliwa na Mhe. Dkt. Jakaya Mrisho Kikwete akiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa wakati wa Awamu ya Pili (2016-2022) ya Kampeni hiyo ambayo ilikuwa na kauli mbiu isemayo NYUMBA NI CHOO ilizinduliwa na Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ambaye alikuwa Makamu wa Rais kwa wakati huo". Amesema Waziri Ummy.

# MKOA WA IRINGA KINARA USHINDI WA JUMLA WA USAFI WA MAZINGIRA

**Na. Hassan Kimweri**
**Kibaha, Pwani**

Mkoa wa Iringa umeibuka kidedea kwa ushindi wa jumla wa usafi na uhifadhi wa mazingira na kuzawadiwa gari aina ya Land Cruiser kwa ajili ya shughuli za Afya Mazingira.

Akitangaza washindi wa usafi na usafi wa mazingira Mei 9, 2024 Kibaha, mkoani Pwani Waziri wa Afya Mhe. Ummy Mwalimu amesema Wizara ya Afya hufanya uhakiki wa vijiji ambavyo vimefikia kiwango cha juu cha usafi, zoezi ambalo linashirikisha vijiji ambavyo kaya zake zote zina vyoo, taasisi zilizopo katika Kijiji hicho na wananchi wa eneo husika wahawajisaidii sehemu zisizo rasmi.

"Mwaka huu tumeongeza kundi moja la Mshindi wa Ujumla kwa Ngazi ya mkoa, ambapo mkoa uliofikia kiwango cha juu cha usafi kwa kuwa na Vijiji vingi vilivyofikia kiwango cha juu cha usafi ni Iringa ambao wanapata zawadi ya gari". Amesema Waziri ummy.

Kwa upande makundi mengine Chuo Kikuu cha Dar Es Salaam kimeibuka mshindi wa kwanza wa usafi na mazingira na kupata cheti na Shilingi Milioni 4, huku Chuo cha Kilimo Sokoine kikiibuka mshindi wa Pili na Chuo cha Sayansi na Teknolojia cha Nelson Mandela kikiambulia ushindi wa Tatu.

Upande wa benki, Benki ya CRDB makao makuu Halmashauri ya jiji la Dar Es Salaam imeibuka mshindi na kupata zawadi ya cheti huku mshindi wa pili ni Benki ya NBC ya jijini Dodoma na mshindi wa tatu ni Benki ya NMB Rock City ya Wilaya na Ilemela jijini Mwanza.

Kundi la Hospitali za Wilaya mshindi wa kwanza ni Hospitali teule ya Migana Wilaya ya Misenyi, mshindi wa pili ni Hospitali ya mji wa Njombe na mshindi wa tatu Hospitali ya wilaya ya Kibosho Wilayani Moshi.

Kundi la Hospitali za Rufaa za Mikoa mshindi wa kwanza ni Hospitali Arusha Lutheran Medical Center (Seriani), mshindi wa pili Hospitali ya Rufaa ya Manyara huku mshindi wa tatu ni Hospitali ya Rufaa ya mkoa wa Arusha ya Mount Meru Arusha.

Kundi la shule za msingi, mshindi wa kwanza ni shule ya Endabash ya wilayani Karatu, mshindi wa pili shule ya Kanikelele iliyopo Halmashuri ya wilaya Njombe huku mshindi wa tatu ni shule ya Idazinyi iliyopo Halmashauri ya Wilaya ya Njombe.






# WAZIRI MKUU MAJALIWA AONGOZA WATANZANIA KWENYE MAZOEZI, KULINDA AFYA

**Na Hassan Kimweri,**
**DAR ES SALAAM**

Waziri Mkuu Tanzania Mhe. Kassim Majaliwa Majaliwa, mapema Mei 4,2024 ameongoza mamia ya Watanzania katika mazoezi afya zao ili kujilinda na Magonjwa Yasiyoyakuambukiza.

Mazoezi hayo yanayoratibiwa na Wizara ya Afya ni moja ya afua iliyo asisiwa na Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan kama moja ya mikakati yakuondokana na maradhi hayo

“Mnakumbuka programu hii iliyoanzishwa na Rais wetu Dkt. Samia Suluhu Hassan na yeye mwenyewe kushiriki na kuwahamasisha watanzania kushiriki mazoezi mbalimbali, katika kipindi cha miaka mitatu ya Dkt. Samia moja ya mambo ya kujivunia ni mafanikio kwenye sekta ya michezo.”

Mheshimiwa Majaliwa ametumia wasaa huo kutoa wito kwa Viongozi wa Manispaa ya Kinondoni kufanya maboresho zaidi katika eneo la fukwe za Coco ili liwe safi na livutie watu wa rika zote.

“Nawapongeza jeshi la polisi kwa kazi nzuri ya ulinzi kwenye eneo hili, Nitoe wito kwenu kuendelea kuimarisha ulinzi ili eneo hili liwe salama kwa watu wa rika na jinsia zote na nyakati zote.”

Awali, Waziri wa Afya Mhe. Ummy Mwalimu amemshukuru Waziri Mkuu kwa kukubali kushiriki katika mazoezi hayo huku akitoa taarifa ya ongezeko la magonjwa 10 yasiyo ya kuambukiza jambo lililofanya Wizara hiyo kuleta ombi la kuanzisha utaratibu wa mazoezi kila jumamosi.

“Mwaka 2022 kati ya magonjwa 10 yaliyotajwa kuwasumbua watanzania moja lililojitokeza ni shinikizo la juu la damu bajeti ya mwaka 2022/2023 likaongezeka na kisukari katika mahlgongwa 10 yanayowasumbua watanzania. Wajibu wa Wizara ya Afya ni kuwakinga Watanzania wasipate magonjwa.”

Kwa upande wake Mkuu wa mkoa wa Dar es Salaam Albart Chalamila amesema kama mkoa watajipanga kuhakikisha utaratibu huo wa mazoezi utakuwa endelevu kwa kishirikiana na kamati ya Ulinzi na usalama pamoja na wadau mbalimbali wa michezo.

Matembezi hayo ya kilomita 10 yalianzia katika fukwe za Coco kupitia daraja la Tanzanite na kumalizikia Ocean Road jijini Dar es Salaam.

# SERIKALI YATOA KIPAUMBELE TAFITI ZA KISAYANSI

**Na Majid Abdulkarim**
**DAR ES SALAAM**

Naibu Waziri Mkuu na Waziri wa Nishati Mh. Dkt. Doto Biteko amesema Serikali itaendelea kufanya utafiti wa ndani ili dawa na chanjo mbalimbali ziweze kuzalishwa nchini huku akiitaka Taasisi ya Taifa ya Utafiti wa Magonjwa ya Binadamu (NIMR) kuimarisha jambo hilo.

Mhe. Biteko ametoa kauli hiyo Mei 14, 2024 Jijini Dar es salaam wakati wa ufunguzi wa Mkutano wa 32 wa Wanasayansi ambao umeandaliwa na NIMR.

Naibu Waziri Mkuu Dkt. Biteko amewahakikishia NIMR pamoja na watafiti wote kuwa Serikali chini ya uongozi wa Rais Samia Suluhu Hassan umewekeza vya kutosha kwenye tafiti hasa kwenye sekta ya afya ili kutatua changamoto kama taifa.

"Pamoja na kwamba tunahitaji watu kutoka nje lakini na sisi wenyewe tuwe na uwezo wa kufanya ugunduzi wa ndani. Amesema na kuongeza

"Tumeishaanza na utaona kuwa zipo hata dawa zenyewe,chanjo zenyewe lazima tuwe na utafiti ambao utatusaidia pengine zizalishwe hapa ndani kwa manufaa ya watanzania na kutufanya kama Taifa ambalo linakuwa kwa kasi kweli kweli,"amesema Biteko

Aidha, Dkt. Biteko amesema maendeleo mahali popote ili yaweze kutokea lazima kuwe na utafiti ambao umebeba ushahidi wa Kisayansi uweze kukupangia wapi unapokwenda na vitu gani utakutana navyo.

Hata hivyo ameongeza kuwa maendeleo yoyote yakifanyika kama hakuna utafiti yatakuwa ni maende ya kubahatisha na matokeo yatakayopatikana yatakuwa ni ya kubahatisha.

"Kutakuwa na kukosea kosea kwingi na matokeo yake rasilimali nyingi zaidi utanitumia.Ndio maana wana Sayansi wanakutana hapa ili kujadili tafiti mbalimbali katika masuala ya afya,"amesema Dkt. Biteko.

Kwa upande wake Naibu Waziri wa Afya, Dkt. Godwin Molel amesema binadamu wote ni sawa lakini miongoni mwao kuna watu wenye uwezo wa kipekee wenye uwezo wa kuona mambo yasiyoonekana kwa macho ya kawaida.

Amesema tofauti ya Mataifa makubwa yaliyoendelea na Mataifa maskini sio ardhi kubwa ama idadi ya watu ni akili za watu hao.



# SERIKALI KUENDELEA KUBORESHA HUDUMA ZA SARATANI NCHINI - DKT. BITEKO



**Na. Eglibert Kayombo**
**DAR ES SALAAM**

Naibu Waziri Mkuu na Waziri wa Nishati, Mhe. Dkt. Doto Biteko amesema Serikali itaendelea kuboresha miundombinu ya utoaji wa huduma za Saratani na vifaa tiba ili kutanua wigo wa huduma za Saratani nchini na hivyo kuwezesha upatikanaji wa huduma hizo kwa urahisi.

Dkt. Biteko amesema hayo Mei 2, 2024 wakati akimwakilisha Rais, Dkt. Samia Suluhu Hassan katika uzinduzi wa Kituo cha Matibabu ya Saratani cha Aga Khan, Jijini Dar es Salaam.

Dkt. Biteko amesema mradi huo wenye thamani ya jumla ya Euro milioni 13.3 (shilingi 35 bilioni) umekuwa na mafanikio mbalimbali ndani ya miaka minne ya utekelezaji wake ikiwemo kutoa mafunzo kwa wahudumu 464 na watumishi 400 ngazi ya jamii kuhusu huduma za saratani.

Kupitia mradi huo wanajamii zaidi ya milioni 4.5 wamepewa elimu kuhusu Saratani, watu takriban laki 700,000 wamepimwa Saratani na zaidi ya wagonjwa wapya 39,093 kugunduliwa kuwa na Saratani kupitia vipimo stahiki na hivyo kuwawezesha kuanza kupata tiba stahiki.

Pia ametoa agizo kwa kituo hicho cha Aga Khan kushirikiana na vituo vingine vya matibabu ya Saratani nchini hususan Taasisi ya Saratani ya Ocean Road ili kuhakikisha kunakuwa na upatikanaji madhubuti wa huduma za tiba za mionzi na hivyo kupunguza msongamano wa wagonjwa Ocean Road.

Awali, Waziri wa Afya, Mhe. Ummy Mwalimu alisema kuwa changamoto ya saratani nchini ni kubwa ambapo kila mwaka kuna wagojwa wapya 40,000 huku vifo 27,000 na kwamba saratani inayoongoza ni ya mlango wa kizazi kwa asilimia 23.5.

Amesema uboreshaji wa huduma za afya nchini unaendelea ili kutimiza dhima ya Rais, Dkt. Samia Suluhu Hassan ya kuhakikisha Tanzania inakuwa kitovu cha utoaji wa huduma za kisasa za Afya kwa wananchi ndani na nje ya nchi.

Kwa upande wake, Mwenyekiti wa Kamati Tendaji ya Taasisi ya Huduma za Afya Aga Khan, Mwana Mfalme Bi. Zahra Aga Khan amesema kujengwa kwa kituo hicho ni ushahidi wa namna Tanzania inavyopiga hatua kwenye Sekta ya Afya kwa kutumia pia teknolojia ya hali ya juu ya kisasa kwenye matibabu.



# MADAKTARI 1,109 KUNUFAIKA NA UFADHILI WA RAIS SAMIA MASOMO YA UBINGWA BOBEZI 2023/24

**Na. Hassan Kimweri**
**DODOMA**

Dkt. Samia Super-Specialized Scholarship Programme imetoa nafasi za ufadhili wa masomo ya ubingwa na ubingwa bobezi ambapo kwa mwaka wa masomo 2023/2024, jumla ya Shilingi 10.9 bilioni zimetengwa na kuwawezesha wanafunzi 1,109 kwenye masomo ya ubingwa na ubingwa bobezi.

Waziri wa Afya Mhe. Ummy Mwalimu amesema hayo Mei 2, 2024 wakati akifungua mkutano wa Mwaka wa chama cha Madaktari bingwa wa magonjwa ya ndani Tanzania (APHYTA) uliofanyika katika ukumbi wa Kinataifa wa Mwalim Julius Nyerere Jijini Dar Es Salaam.

"Serikali imeendelea kutoa kipaumbele kwa madaktari bingwa kwa kuwaendeleza kitaaluma kupitia programu ambayo imetoa nafasi za ufadhili wa masomo ya ubingwa kwa mwaka wa Masomo 2023/2024, kwa wanafunzi 1,109 ikiwa ni ongezeko la wanafunzi 582 ukilinganisha na mwaka wa masomo 2022/2023." Amesema Waziri Ummy

Amesema, idadi ya wanafunzi wote ambao wamepata ufadhili kupitia programu hiyo, wanafunzi 79 watasomea udaktari bingwa wa magonjwa ya ndani na kati yao madaktari 11 sawa na asilimia 33 wamekwenda kusoma ubingwa bobezi wa magonjwa ya ndani.

Aidha, Waziri Ummy ametoa wito kwa madaktari vijana kujitokeza kwa wingi kwenda kujiendeleza katika masomo ya ubingwa bobezi hususan kwenye magonjwa ya ndani na wakirudi wakubali kupangiwa sehemu yoyote kwa kuwa Mikoa mingine pia inahitaji madaktari bingwa bozezi.

"Kupitia muundo huu mpya wa Sekta ya Afya, tutaweza kuwatambua kwa kuwawekea mazingira mazuri madaktari wenye Ubobezi katika maeneo mbalimbali ikiwemo wa masuala ya magonjwa ya ndani." Amesema Waziri Ummy

Katika hatua nyingine Waziri Ummy amewataka madaktari hao kujadiliana na kuja na mapendekezo ya jinsi ya kupunguza magonjwa Yasiyoambukiza kwa kuwa kwa sasa kumekuana ongezeko kubwa la magonjwa hayo.

Pia, Waziri Ummy amewataka madaktari hao kujadiliana na kutoa maoni yao katika muongozo wa Kitaifa wa matibabu pamoja na orodha ya Taifa ya dawa ili kama kuna mapungufu yaweze kurekebishwa.

# MADAKTARI BINGWA WA RAIS SAMIA WATASAIDIA KUPUNGUZA VIFO VYA WATOTO WACHANGA

**Na Hassan Kimweri**
**IRINGA**

Mpango kabambe wa madaktari bingwa wa Dkt. Samia utasaidia kupunguza vifo vya watoto wachanga kwa kuwajengea uwezo watoa huduma wengine katika Hospitali za Halmashauri kwa kuwa dhamira ya Serikali ni kuwa na wodi maalum za watoto wachanga (NCU) katika Hospitali hizo ili kuokoa maisha ya watoto wachanga wenye siku 0-28.

Waziri wa Afya Mhe. Ummy Mwalimu amesema hayo Mei 6, 2024 wakati akizundua Mpango kabambe wa utoaji wa huduma za Kibingwa kwenye Hospitali 184 katika ngazi ya Halmashauri zinazofanywa na Madaktari bingwa wa Dkt. Samia yenye kauli mbiu isemayo "Tumekufikia, Karibu Tukuhudumie".

"Nasisitiza tena kwamba, sambamba na utoaji huduma na kujenga uwezo wa watoa huduma wetu, Madaktari bingwa saidieni uanzishaji na kuimarisha utendaji wa NCU kwa kuwa katika mpango huu mtafikia Hospitali zote za Halmashauri." Amesisitiza Waziri Ummy

Waziri Ummy ameongeza kuwa kila mwanamke mjamzito anayefika Hospitali kwa ajili ya kujifungua anatakiwa atoke salama yeye na kichanga chake.

"Tunaweza kuokoa maisha ya watoto wachanga endapo tutaanzisha wodi maalum za watoto wachanga, tukaviwekea vifaa tiba ili endapo mtoto akiwa na changamoto yoyote aweze kupata huduma". Amesisitiza Waziri Ummy.

Aidha, Waziri Ummy amesema Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan ameweka rekodi Duniani kwa kupunguza vifo vitokanavyo na uzazi kwa asilimia 80, kutoka vifo 556 kati ya vizazi hai 100,000 mwaka hadi vifo 104 kati ya 100,000 takwimu za mwaka 2020/2022.

Waziri Ummy ametoa wito kwa viongozi wa Mikoa na Halmashauri kufanya kazi kwa karibu na ushirikiano wa hali ya juu kwa madaktari bingwa wa Rais Samia kwa kuwa wamekuja hapa kutoa huduma kwa wananchi.

Kwa upande wake Mkurugenzi Msaidizi wa huduma za mama na mtoto Dkt. Felix Bundala amesema katika siku Tano Mikoa ya Tanga, Songea pamoja na Geita wamefikiwa wateja 6,381.

"Kati ya wateja 6,381 walioonwa, waliofanyiwa upasuaji ni 166 sawa na 3% waliopewa rufaa ni 42 ambao ni sawa na mtu Mmoja katika watu 100 amepata rufaa." Amesema Dkt. Bundala.






# TUTAZIDI KUIMARISHA HUDUMA ZA UKUNGA KUKABILINA NA VIFO VITOKANAVYO NA UZAZI

**Na Hassan Kimweri**
**DAER ES SALAAM**

Serikali kupitia Wizara ya afya imedhamiria kuendelea kuboresha huduma za Ukunga sambamba na kuongeza idadi yao ili kupunguza vifo vya watoto wa mchanga.

Waziri wa Afya Mhe. Ummy Mwalimu amesema hayo Mei 5, 2024 kwenye siku ya Mkunga duniani ambapo mgeni rasmi katika Maadhimisho hayo alikuwa Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mhe. Kassim Majaliwa.

"Uwepo wa Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mhe. Kassim Majaliwa katika Maadhimisho haya ni kielelezo kuwa Serikali ipo tayari kujenga na kuweka mazingira mazuri ya kufanya kazi kwa wakunga ikiwa ni njia moja wapo ya kupunguza vifo vitokanavyo na uzazi." Amesema Waziri Ummy

Amesema, sio kila mtu anaweza kufanya kazi ya ukunga, ukunga ni taaluma ambayo tunataka tuendelee kuitambua zaidi na wakati umefika wa kutofautisha Uuguzi na Ukunga.

Aidha, Waziri Ummy amesema wakunga wamekuwa msaada mkubwa kwenye kupungua kwa vifo vitokanavyo na uzazi na vifo vya watoto wachanga ambapo afua nyingi za afya za uzazi na mtoto zinaendelea kuboreshwa ili kutoa huduma bora za uzazi na afya ya mtoto.

"Serikali imeongeza upatikanaji wa huduma za uzazi salama, huduma za uzazi wa mpango, upimaji wa Virusi vya UKIMWI (VVU) kwa wajawazito, upimaji wa Saratani ya mlango wa kizazi, utoaji wa chanjo kwa rika zote pamoja na utolewaji wa elimu ya afya ya uzazi." Amefafanua Waziri Ummy

Waziri Ummy amemshukuru Mhe. Rais kwa kuiwezesha Sekta ya Afya katika kuboresha huduma za Afya hususan Afya ya Uzazi mama na mtoto ambapo vifo vya wajawazito vimepungua kwa 80%.

Katika hatua nyingine Waziri Ummy amewataka wakunga hao kuendelea kuwahudumia wateja kwa kutambua wajibu wao wa kuimarisha afya zao ili kufanikisha Dira ya 2025 ya Tanzania na Mende Endelevu yenye malengo kupitia utoaji wa huduma ya afya ya uzazi inayokidhi mahitaji ya afya ya uzazi kwa wanawake na vijana.

# TANZANIA YAPENDEKEZA KUNZISHWA KWA VITUO VIWILI VYA UMAHIRI KWA NCHI ZA AFRIKA MASHARIKI



**Na Hassan Kimweri**
**DAR ES SALAAM**

Serikali kupitia Wizara ya Afya imetoa mapendekezo kwa Baraza la Mawaziri wa Kisekta wa Afya wa Jumuiya ya Afrika Mashariki (EAC) lipitishe maombi ya Tanzania kuanzisha vituo viwili vya umahiri kwa Afrika Mashariki vitakavyotoa huduma za Afya ya Kinywa na Meno pamoja na huduma za upandikizaji Uloto.

Waziri wa Afya Mhe. Ummy Mwalimu amesema hayo Mei 3, 2024 kwenye Mkutano wa 24 wa Baraza la Mawaziri wa Kisekta wa Afya wa Jumuiya ya Afrika Mashariki (EAC) uliofanyika Jijini Dar Es Salaam ambapo Makatibu Wakuu na Manaibu Katibu Wakuu wamehudhuria.

"Chuo Kikuu cha Muhimbili kupitia idara ya kinywa na meno ina wataalamu wa kutosha pamoja na vifaa, kwa hiyo tunataka wataalamu wote wa kinywa na meno wa Afrika Mashariki waje Tanzania kujifunza katika Taasisi yetu ya MUHAS." Amesema Waziri Ummy

Waziri Ummy amesema Tanzania inafanya vizuri katika masuala ya upandikizaji viungo ikiwemo upandikizaji wa Uloto hususan kwa watoto wenye changamoto za Sikoseli ambayo ni kati ya nchi Tano Duniani yenye idadi kubwa ya watoto wanaozaliwa na Sikoseli.

Aidha, Waziri Ummy amesema katika Mkutano huo wameweza kujadili kuhusu magonjwa Yakuambukiza ambapo kwa Bara la Afrika Mashariki inakabiliwa na changamoto za magonjwa ya Malaria, UKIMWI pamoja na Kifua Kikuu pamoja na magonjwa Yasiyoambukiza.

Amesema, ili kuepuka magonjwa Yasiyoambukiza ni kuzingatia ulaji wa vyakula, kupuguza unywaji wa pombe na ufanyaji wa mazoezi, kwa Tanzania kila siku ya Jumamosi kuanzia saa 12:00 asubuhi hadi saa 3:00 asubuhi imetengwa kuwa ni muda wa mazoezi ambapo Waziri Mkuu alitoa agizo la kufungwa na Daraja la Tanzanite kwa muda huo ili kuwapa uhuru watu wanaofanya mazoezi.

Kwa upande wake, Katibu Mkuu Wizara ya Afya Kenya Bi. Mary Muthoni amesema Jamii inapaswa kuelimisha juu ya Afya kwakuwa Afya inaanzia nyumbani, "usipokata vichaka shida inaanzia nyumbani, usipokula vizuri shida inaanza nyumbani, usipoweka maji safi na salama shida inaanzia nyumbani".




# TRILION 1.3 KUTEKELEZA VIPAUMBELE 10 VYA WIZARA YA AFYA

**Na Shaban Juma**
**DODOMA**

Wizara ya Afya imepanga kutekeleza vipaumbele 10 kwa kutumia afua 86 zinazokadiriwa kutumia kiasi cha shilingi 1,311,837,466,000 kwa mwaka ujao wa fedha 2024/25 itakayohusisha mapato, matumizi ya kawaida na miradi mbalimbali ya maende kwa mwaka huo

Hayo yamebainishwa Jumatatu Mei 13.2024 na Waziri wa Afya Mhe. Ummy Mwalimu wakati akiwasilisha Hotuba ya makadirio ya mapato na matumizi ya Wizara hiyo kwa mwaka wa fedha 2024/25 Bungeni jijini Dodoma kupitia Bunge la 12, Mkutano wa 15, Kikao cha 24 ambapo ametaja vipaumbele hivyo kuwa ni pamoja na kuimarisha huduma za kinga dhidi ya magonjwa ambapo katika eneo hilo kiasi cha shilingi 117, 611,588,304 kimetengwa

Vipaumbele vingine ni pamoja na kuimarisha upatikanaji wa ubora wa huduma za afya zinazotolewa na vituo vya kutolea huduma za afya katika ngazi zote ambapo jumla ya shilingi 219,010,767,716 zimetengwa ili kutekeleza eneo hilo, sambamba na hilo liko suala la kuimarisha huduma za afya za uzazi, mama na mtoto ambapo kwenye eneo hilo kiasi kilichotengwa ni shilingi 17,189,250,000

Waziri Ummy ametaja vipaumbele vingine kuwa ni pamoja na kuimarisha upatikanaji wa wataalam katika sekta ya afya katika fani za kati, ubingwa na ubingwa bobezi ambapo kwenye eneo hilo kiasi kilichotengwa ni shilingi 74,000,000,000, hiyo ikienda sambamba na kuimarisha huduma za matibabu ya ubingwa na ubingwa bobezi nchini ambapo kiasi kilichotengwa kwenye eneo hilo ni shilingi 89,858,609,000

Aidha, katika vipaumbele hivyo lipo suala la kuendeleza na kusimamia afua za Tiba Asili na Tiba Mbadala ambapo kiasi cha shilingi 1,500,000,000 kimetengwa, kuimarisha udhibiti wa magonjwa ya kuambukiza, magonjwa yasiyoambukiza, magonjwa ya mlipuko na huduma za afya za dharura ambapo kwenye eneo hilo Wizara imetenga kiasi cha shilingi 84,864,241,569, na kuimarisha huduma za afya ya akili ambapo kiasi kilichotengwa kwenye eneo hilo ni shilingi 5,618,528,988

Pia, Wizara ya Afya imegusia suala la kuimarisha huduma za utengamao na tiba shufaa hususani kwa watoto, wazee na wenye ulemavu ambapo kiasi kiasi cha shilingi 3,700,000,000 kimetengwa kwenye eneo hilo

Vipaumbele vingine vilivyowekwa na Wizara ya Afya kwa mwaka ujao wa fedha ni pamoja na kusimamia tafsiri na matumizi ya matokeo ya tafiti mbalimbali za afya ambapo kiasi kilichotengwa ni shilingi 3,508,968,000, pamoja na kuimarisha mifumo ya ugharamiaji wa huduma za afya nchini ambapo kiasi kilichotengwa kwenye eneo hilo ni shilingi 6,000,000,000

# ROBOT KUTUMIKA KATIKA UPASUAJI WA UBONGO NA MISHIPA YA FAHAMU

**Na Aisha Swahibu**
**DODOMA**

Waziri wa Afya Mhe. Ummy Mwalimu amesema Serikali imekusudia kuanzisha huduma mpya za upasuaji wa ubongo na mishipa ya fahamu kwa kutumia akili mnembo (ROBOT) katika Taasisi ya Taifa ya Mifupa MOI

Akizungumza wakati wa uwasilishaji wa Bajeti ya makadirio ya mapato na matumizi ya Wizara ya Afya kwa mwaka wa fedha 2024/25 Bungeni jijini Dodoma  Jumatatu Mei 13, 2024 ambapo amesema serikali inakwenda kuandika historia hiyo (ya kufanya upasuaji kwa kutumia Robotic surgery) katika Taasisi ya Taifa ya mifupa (MOI)

Sambamba na hilo Waziri Ummy amesema Hospitali ya Kanda Bugando pia inakwenda kuanzisha huduma za upandikizaji wa figo, wakati Hospitali ya Taifa Muhimbili na Hospitali ya Benjamin Mkapa ziko mbioni kuanzisha huduma ya upandikizaji wa ujauzito

Waziri Ummy amesema wanawake wengi wamekuwa wakitamani kupata mtoto/watoto lakini wanashindwa kumudu gharama kutokana na kwamba baadhi ya Hospitali binafsi zinazotoa huduma hizo zimekuwa zikiweka kiwango cha juu cha gharama, hivyo hatua ya huduma hizo kutolewa kwenye Hospitali za umma itapelekea wanawake wanye matamanio hayo kupata huduma hizo kwa gharama nafuu

Aidha, katika Hospitali ya Rufaa ya Kanda Mbeya Serikali kupitia Wizara ya Afya inakusudia kununua mtambo wa Cathlab utakaofanikisha kufanyika kwa upasuaji wa moyo bila kufungua kifua, huduma kama hiyo pia itapatikana kwenye Hospitali ya Rufaa ya Kanda Chato

Katika hatua nyingine Waziri Ummy amesema Taasisi ya Saratani ya Ocean road inakwenda kuanzisha kituo cha Saratani Mbeya, wakati Taasisi ya moyo ya Jakaya Kikwete iko mbioni kufungua tawi la huduma hiyo kwenye Hospitali ya Kanda Chato kwa ajili ya wakazi wa maeneo ya Kanda ya Ziwa na viunga vyake



# ASILIMIA 92 YA WASICHANA WENYE UMRI WA MIAKA 14 WAMEPATA CHANJO YA HPV



**Na Aisha Swahibu**
**DODOMA**

Serikali imeendelea kuwalinda wasichana wenye umri wa miaka 14 dhidi ya Saratani ya mlango wa kizazi kwa kununua na kusambaza chanjo ya Human Papilloma Virusi (HPV) kulingana na mahitaji ya chanjo hiyo hapa nchini.

Waziri wa Afya Mheshimiwa Ummy Mwalimu amesema hayo Bungeni Mei 13, 2024 akiwa anawasilisha hotuba yake ya bajeti ya Wizara ya Afya kwa mwaka wa fedha 2024/25 akielezea utekelezaji wa majukumu ya Wizara katika utoaji wa huduma za Kinga nchini.

"Hadi kufikia mwezi Machi 2024 jumla wasichana 663,949 walikuwa wamepatiwa chanjo ya HPV sawa na asilimia 92 ya walengwa ikilinganishwa na Wasichana 535,708 waliopata chanjo hiyo kwa kipindi kama hicho mwaka 2022/2023." Amesema Waziri Ummy

Waziri Ummy Mwalimu amesema lengo lilikuwa ni kuchanja jumla ya wasichana laki 721,684 wenye umri wa miaka 14 kwa ajili ya chanjo ya HPV ili kuwakinga wasichana hao dhidi ya Saratani ya mlango wa kizazi.

"Chanjo ni moja ya njia zilizothibitika kisayansi kuzuia magonjwa, hivyo nichukue fursa hii kuwahimiza wananchi hususan wazazi/walezi wenye watoto wa umri chini ya miaka mitano (5) kuendelea kuchukua tahadhari dhidi ya magonjwa yanayozuilika na chanjo kama inavyoshauriwa na wataalam wa afya." Amesema Waziri Ummy




# DKT. MOLLEL AONYA VIKALI MAAFISA UTUMISHI KUINGILIA MAJUKUMU YA MAKATIBU WA AFYA

**Na Majid Abdulkarim**
**ARUSHA**

Naibu Waziri wa Afya Dkt Godwin Mollel amewaasa makatibu wa Afya nchini kufanya kazi kwa kujiamini, Uadilifu na Ueledi kwa kuzingatia Miongozo na Kanuni na taratibu zilizopo ili kuepusha migongano na malalamiko katika taasisi walipo.

Dkt. Mollel ameitoa kauli hiyo Jijini Arusha wakati akimwakilisha Naibu Waziri Mkuu Dkt Dotto Biteko kwenye ufunguzi wa Mkutano Mkuu wa Mwaka wa Chama cha Makatibu wa Afya Nchini.

Dkt. Mollel amesema Makatibu wa Afya ngazi zote za kutolea huduma za afya wameleta mafanikio na mabadiliko makubwa ndani ya sekta ya afya nchini.

"Hivi sasa idadi ya vyuo vinavyotoa mafunzo ya Kada ya Makatibu wa Afya imeongezeka ikiwa ni kielelezo cha umuhimu wa kada hiyo katika vituo vya kutolea huduma za afya nchini" amesema Mollel.

Wakati huo huo Dkt. Mollel ameilekeza Wizara ya afya kubainisha wazi majukumu ya Maafisa utumishi na Makatibu wa Afya kwenye Hospitali za Rufaa za Mikoa ili kuzuia migongano katika utendaji.

"Jambo hili lichukuliwe kwa uzito na utatuzi wa haraka kwani kada zote hizi ni muhimu hivyo, misuguano yao inaleta madhara makubwa kwa watumishi na wagonjwa wanaoenda kupata huduma kwenye taasisi hizi,"amesema Dkt.Mollel.

Dkt.Mollel amesema Makatibu wa Afya ndio wasimamizi wa rasimali na nyenzo za kutolea huduma za afya hivyo wanatakiwa kufanya maandalizi ya kutoa elimu kwa wananchi juu ya Bima ya Afya kwa Wote ili utekelezaji ukianza ulete matokeo bora.



# WATAALAMU WA VINASABA TUMIENI TEKNOLOJIA KWENYE MAJUKUMU YENU: DKT. JINGU

**Na Abdulwaheed Madenge**
**DODOMA**

Katibu Mkuu wa Wizara ya Afya, Dkt. John Jingu, ametoa rai kwa kamati ya kitaalamu wanaofanya uchunguzi wa Vinasaba vya Binadamu kuzingatia matumizi ya teknolojia huku wakizingatia weledi na kufuata maadili ya kazi ili kuepuka madhara au migogoro inayoweza kujitokeza.

Dkt. Jingu amesema hayo 6 Mei, 2024 jijini Dodoma wakati akizindua Kamati ya kitaalamu ya Vinasaba vya Binadamu ikiwa ni sehemu ya utekelezaji wa Sheria ya Vinasaba vya Binadamu Sura ya 73 inayo ongozwa na Mwenyekiti wake ambaye pia ni Mganga Mkuu wa Serikali Prof. Tumaini Nagu.

Katibu Mkuu Dkt. Jingu amesema serikali ina imani na kamati hiyo kwani itasaidia Mamlaka ya Maabara ya Mkemia Mkuu wa Serikali kutimiza wajibu wake kwa nchi na Serikali na kuendeleza mahusiano mema na Taasisi ambazo zina majukumu yanayoshabihiana.

"Ni matumani yangu kuwa kamati tunayoizindua hii itasaidia Mamlaka ya Maabara ya Mkemia Mkuu wa Serikali kutimiza wajibu wake kwa nchi na Serikali, lakini pia itaendeleza mahusiano mema ya kiutendaji kati ya Mamlaka hii na taasisi ambazo zina majukumu yanayoshabihiana". Amesema Dkt Jingu.

Katibu Mkuu huyo ameongeza kuwa, Masuala ya Vinasaba yana mambo mengi ambayo yanaweza kuisaidia jamii, lakini pia yanahitaji kiwango kikubwa cha kimaadili na kiusimamizi, hivyo amewataka wataalam kufanya kazi kwa weledi na kwenda sambamba na mabadiliko ya teknolojia ya vinasaba kwa kuwa dunia inabadilika kwa haraka kila siku.

Kwa upande wake Mkemia Mkuu wa Serikali Dkt. Fidelice Mafumiko, ametaja majukumu ya msingi yanayofanywa na Mamlaka ikiwemo sheria ya Udhibiti Matumizi ya Vinasaba vya Binadamu sura ya 73.

# WAZAZI TENGENI BAJETI YA YA KUWANUNULIA TAULO ZA KIKE WATOTO WENU WA KIKE

**Na Atley Kuni**
**ARUSHA**

Wazazi na walenzi nchini wametatakiwa kuhakikisha wanawawezesha watoto wa kike kila mwezi kupata vifaa vyao vyakujilinda na kuwa na hedhi salama katika muda husika.

Rai hiyo imetolewa Mei 28, 2024 na Naibu Waziri wa Afya, Dkt. Godwin Molel wakati akizungumza kwenye kilele cha maadhimisho ya juma la hedhi Salama Duniani ambayo Kitaifa yameadhimishwa Jijini Arusha.

Wazazi mara nyingi tumekuwa tukitenga bajeti ya kununua vitu mbalimbali kwa ajili ya matumizi majumbani kwetu lakini eneo hili la kununua pedi ‘taulo za kike’ mara nyingi tunakuwa tunalisahau, niwaombe Wazazi na walezi wote tutenge bajeti ya kila mwezi kwa ajili ya kuwezesha hawa mabinti zetu waweze kuwa na uhakika wa kuwa na taulo za kike na kufikia malengo ya hedhi salama” amesema Naibu Waziri Dkt. Mollel.

Dkt Molel amesema Serikali imekuwa ikihimiza uwekezaji wa uzalishaji bidhaa za hedhi nchini ili ziweze kupatikana kwa urahisi na kwa gharama nafuu. Hata hivyo amepongeza mchango wa wadau wa Sekta katika kuweka mazingira rafiki ya upatikanaji wa taulo hizo.

"Napenda kutoa pongezi kwa Kiwanda cha A-Z kilichopo hapa Arusha kwa kuanzisha uzalishaji wa bidhaa hizi muhimu nchini ambapo kwa sasa wanazalisha taulo za kike zitakazo weza kutumika kwa muda mrefu,"amesema Dk Mollel huku akiwaomba wazalishaji wengine kujitokeze kuwekeza kwenye uzalishaji wa bidhaa za hedhi ili ziweze kupatikana kwa wingi na kwa gharama nafuu nchini.

Akisoma taarifa ya Jukwaa la Hedhi Salama nchini Bi. Mariam Mashimba ambaye ni Mwenyekiti wa Jukwaa hilo amesema hivi sasa watumiaji wengi katika shule wanapendelea taulo zakufua.

"Wakati wa utafiti asilimia 75% ya wanafunzi waliohojiwa katika baadhi ya shule za sekondari na msingi ndani ya mikoa 22 ambako utafiti ulifanyika walionesha kupendelea zaidi taulo za kufua kwani huokoa uchumi wa wazazi wao na kutunza mazingira lakini pia huondokana na adha ya kukosa mahali pa kutupa pindi wanapomaliza kutumia" amesema Bi Mashimba.



# WAGONJWA WAPYA WA SARATANI 40 ELFU HUGUNDULIKA KILA MWAKA, VIFO 27 ELFU

**Na. Hassan Kimweri**
**DAR ES SALAAM**

Waziri wa Afya Mhe. Ummy Mwalimu amebainisha kuwa takribani wagonjwa wapya wa Saratani 40,000 hugunduliwa kila mwaka na karibu jumla ya watu 27,000 wenye Saratani hufariki dunia nchini Tanzania.

Waziri Ummy amesema hayo Mei 2, 2024 kwenye uzinduzi wa jengo la huduma za Saratani lililopo Hospitali ya Aga Khan iliyozinguliwa na Naibu Waziri Mkuu na Waziri wa Nishati, Mhe. Dkt. Doto Biteko ambapo kituo hicho kitatoa huduma kwa wagonjwa 100 kwa siku.

"Takwimu za ufuatiliaji wa Saratani kupitia ripoti ya utafiti ya Globocan zinaonesha kuwa nchini Tanzania takribani wagonjwa wapya wa Saratani elfu 40 hugunduliwa kila mwaka na karibu jumla ya watu elfu 27 wenye Saratani hufariki dunia kila mwaka kutokana na ugonjwa huu." Amesema Waziri Ummy

Amesema, sehemu kubwa ya wagonjwa wa Saratani hapa nchini wamebainika kuwa ni wanawake wenye Saratani ya mlango wa kizazi ambapo Saratani hii pekee inachangia 25% ikifuatiwa na Saratani ya matiti kwa 10% ambapo kwa pamoja Saratani hizi zinachangia zaidi ya 33% ya wagonjwa wote na kwa pamoja zinachangia karibu nusu ya vifo vyote vinavyotokana na Saratani hapa nchini.

"Vifo vitokanavyo na Saratani vitaongezeka ifikapo mwaka 2030 kama hatutachukua hatua za kushuhulikia ukubwa wa tatizo hili la Saratani nchini ambapo inakadiriwa kufikia vifo Milioni Moja kwa Mwaka 2030." Amesema Waziri Ummy

Waziri Ummy amesema Serikali kupitia Wizara ya Afya inaendelea na mapambano dhidi ya Saratani ambapo amesema fedha imepatikana ya kuboresha miundombinu, ununuzi wa vifaa vya kisasa pamoja na kusomesha wataalam katika matibabu ya Saratani.

"Tunamshukuru Mhe. Rais Samia ametupatia Bilioni 10 Mwaka huu, tumesomesha madaktari bingwa na bozezi kwenye masuala ya Saratani zaidi ya 30 ambao tumewapeleka nje ya nchi ambao watakuja kusaidia kupunguza tatizo la Saratani nchini." Amesema Waziri Ummy






# WAUGUZI MSINGI WA HUDUMA BORA ZA AFYA: DKT. MOLLEL

**Na Majid Abdulkarim**
**TANGA**

Serikali kupitia Wizara ya Afya, imewapongeza Wauguzi nchini kwa kujitoa na utayari wao wa kutoa huduma bora, zenye staha na zinazojali utu.

Pongezi hizo zimetolewa Mei 12, 2024 Jijini Tanga na Naibu Waziri wa Afya, Dkt. Godwin Mollel wakati wa maadhimisho ya siku ya Wauguzi Duniani ambapo Naibu Waziri Mkuu Dkt Dotto Biteko amemwakilisha Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Dkt Samia Suluhu Hassan.

Dkt.Mollel ambaye pia ni Mbunge wa Siha amesema katika siku hiyo maalum ya kusheherekea siku ya Wauguzi Duniani, wanatambua na kusherehekea mafanikio makubwa ya wauguzi.

Pia amethibitisha dhamira ya Serikali kufanya kazi pamoja ili kujenga mustakabali wenye afya na usawa zaidi kwa wote.

“Tunasema asante kwa wauguzi kwa kuji toa kwenu na utayari wenu wa kutoa huduma bora zenye staha na zinazojali utu”amesema Dkt.Mollel

Hata hivyo amewasihi Wauguzi nchini waendelee kuwahudumia wateja kwa kuzingatia miiko ya taaluma yao.

"Huku mkitambua wajibu mlio nao katika kuimarisha afya za watanzania.Nawapongeza sana wauguzi wote wa Tanzania kwa kazi kubwa na nzuri mnazofanya,"amesema Dkt.Mollel

# HOSPITALI ZATAKIWA KUIMARISHA KARAKANA ZA VIFAA TIBA ILI KUSAIDIA KATIKA UTOAJI WA HUDUMA ZA UHAKIKA

**Na Shaban Juma**
**DODOMA**

Katibu Mkuu wa Wizara ya Afya, Dkt. John Jingu amewata Waganga Wafawidhi wa Hospitali nchini kuimarisha karakana za vifaa tiba katika hospitali zao ili ziweze kutengeneza vifaa vitavyoharibika.

Dkt. Jingu amesema hayo  Mei 7, 2024 Jijini Dodoma wakati akipokea vifaa vya hewa tiba ya Oxygen vilivyotolewa na Shirika la Clinton Health Access Initiative (CHAI) ambalo linajishughulisha na masuala ya kutengeneza vifaa tiba katika baadhi ya Hospitali nchini.

Vifaa vilivyotolewa na Shirika hilo ni pamoja na Handheld Pulse Oximeters, Oxygen analyzers na Oxygen Wall- Flowmeters (Complete sets) ambavyo vitapelekwa katika Hospitali za Rufaa za Mikoa ya Sekoue Toure, Hospitali ya Rufaa ya Mkoa Singida, Hospitali ya Rufaa ya Mkoa Dodoma pamoja na Hospitali ya Rufaa ya Kanda ya Mbeya.

Dkt. Jingu amesema ili vifaa hivyo viweze kudumu na kutoa huduma kwa wananchi ni lazima vifanyiwe matengenezo hivyo Hospitali zilizopata vifaa ni ziimarishe karakana ili waweze kutengeneza vifaa tiba hapa hapa nchini.

Aidha, Dkt. Jingu amesema Serikali ya Rais Samia imewekeza kwenye vifaa tiba kuanzia katika Zahanati hadi Hospitali kubwa ambazo zinawawezesha watoa huduma kutoa huduma bora zinazochagizwa na uwepo wa vifaa tiba vya kisasa.

"Tunajenga uwezo kwa wataalamu wa karakana ili waweze kutengeneza vifaa tiba vilivyo chakavu vinavyohitaji marekebisho sambamba na kutengeneza vifaa vyetu wenyewe, tuna Kanda saba kila Hospitali na kituo wote wana wataalamu wao wa kufanyia matengenezo". Amesema Dkt. Jingu.

"Ndio maana ndugu zetu wa CHAIi tunawashukuru sio tu kwa vifaa vya hewa tiba mlivyotoa bali vifaa vyote vya uchunguzi ikiwemo X- ray tutengeneze humu humu kwa kuwatumia wataalam wetu waliojengewa uwezo". Ameongeza Katibu Mkuu huyo.

Dkt. Jingu ameendelea kutoa wito kwa wadau kuendelea kushirikiana na Serikali ya Rais Samia Suluhu Hassan kwani sekta binafsi ina umuhimu mkubwa katika kuboresha huduma za afya nchini.





# WAGANGA WAFAWIDHI, MADAKTARI BINGWA WATAKIWA KUENDELEA KUVIISHI VIAPO VYAO

**Na. Cletus Sanga**
**DODOMA**

Waganga Wafawidhi na Madaktari Bingwa wametakiwa kuendelea kuviishi viapo vyao kwa kutambua dhamana Kubwa waliyoibeba katika kuisaidia Serikali kufikisha huduma bora za afya kwa jamii na kutoa Huduma bora kwa watanzania.

Ukumbusho huo umetolewa na Mganga Mkuu wa Serikali Prof. Tumaini Nagu wakati akizungumza na Waganga Wafawidhi wa Hospitali za Rufaa za Mikoa na Madaktari Bingwa  tarehe 14 Mei, 2024 Jijini Dodoma.

Prof. Nagu amesema Serikali inatambua Kazi kubwa wanayoifanya Madaktari hao na kuongeza kuwa kada ya Udaktari ni wito na kazi iliyo karibu zaidi na Mwenyezi Mungu hivyo amewataka Madaktari hao kukumbuka Viapo vyao.

"Tunaposema huduma za Afya tunamaanisha Matibabu, kinga, utengamao na elimu ya afya kwa umma hivyo ni wajibu wenu kuhakikisha watanzania wanapata huduma za kinga, na elimu juu ya afya zao Kwa wakati. Serikali kwakutambua kazi kubwa mnayoendelea nayo, nawakumbusha kuendelea kuviishi viapo vyenu hasa kwa kutambua pia hii ni kazi kiimani pia sio maslahi pekee" Amesisitiza Prof. Nagu

Prof. Nagu ameongeza kuwa zaidi ya asilimia 70 hadi 80 watanzania wanapata huduma za afya kwa ngazi ya msingi hii ni kutokana na uwekezaji wa Serikali kwenye sekta ya Afya na kuwataka Waganga Wafawidhi hao kuendelea kuboresha utoaji wa huduma kwenye Hospitali zao.

"Niwashukuru na kuwapongeza kwa Kazi nzuri na kubwa mnayoifanya , Pamoja na changamoto mbalimbali na mazingira magumu mnayokutana nayo lakini bado mmekuwa mkifanya kazi kubwa kwa weledi Serikali na Wizara ya Afya inatambua mchango wenu na tutazidi kuwapa ushirikiano kwa kila namna mtakavyotuhitaji" ameongeza Prof. Nagu.

Katika kuhitimisha Mganga Mkuu wa Serikali Prof. Nagu amewataka Waganga Wafawidhi hap kuzingatia Mambo matatu, Mawasiliano mazuri na wagonjwa, Utoaji wa huduma bora kwa Mteja na Kufuta miongozo katika uharaka wa utoaji wa huduma kuzingatia utoaji wa dawa na Matibabu.



# TANZANIA YAWEKA BAYANA UBUNIFU UNAOFANYIKA KUFIKIA AFYA KWA WOTE

**Geneva Uswisi**

Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kupitia Wizara ya Afya imeweka bayana mikakati na ubunifu unaofanyika kufikia malengo ya Afya kwa wote ifikapo 2030

Akizungumza wakati wa Mkutano wa pembezoni Mei 28,2024, jijini Genive Uswis, Waziri wa Afya Mhe. Ummy Mwalimu amesema kama nchi shabaha yao ni ifikapo 2030 lazima lengo hilo liwe limetimia.

"Kwa nchi za Afrika tukiongeza ubunifu unaofanywa na nchi zetu kwenye kuongeza wigo wa kutoa huduma za Afya na ugharimiaji malengo yetu yatatimia" amesema Mhe. Ummy

Waziri Ummy amefafanua kuwa maeneo ya ubunifu yaliyowasilishwa ni pamoja na Jukwaa la Wadau wa Sekta ya Afya lililofanikisha kuanzishwa kwa Mfuko wa pamoja wa Afya ambao umewezesha kuimarika kwa utoaji huduma kwa ngazi ya msingi.

Ummy ameongeza kwamba eneo lingine ni ushirikiano na mashirika ya Kimataifa ni Global Fund, PEPFAR, USAID na CDC ambayo yameiwezesha Tanzania kuimarisha mifumo ya Afya ikiwemo kuongeza rasilimali fedha ili kukabiliana na magonjwa ya kuambukiza na yasiyo ya kuambukiza.

"Kupitia ushirikiano kati ya sekta binafsi, Tanzania tumeweza kusogeza huduma za afya karibu na wananchi" amefafanua Waziri Ummy

Mjadala huo umefanyika pembezoni mwa kikao 77 cha Shirika la Afya Duniani kinachoendelea Geneva, Uswisi na kuwakilishwa Tanzania imewakilishwa
na Mhe Ummy Mwalimu (Mb), Waziri wa Afya wa Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Mhe Nassor Mazrui (Mb), Waziri wa Afya, Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar



# ALIYETESEKA KWA MIAKA 10 NA MAWE KWENYE KIBOFU AFANYIWA UPASUAJI

**Na Cletus Sanga**
**KONDOA, DODOMA**

Madaktari bingwa wa Rais Samia wamefanikiwa kutoa mawe kwenye kibofu cha mkojo cha Bw. nard Mhunda Mkazi wa Chamwino Mkoani Dodoma ambayo yalimtesa kwa takriban miaka 10.

Akizungumza mara baada ya kumfanyia upasuaji na kumtolea Mawe kwenye kibofu Daktari Bingwa wa upasuaji Dkt. Tito Lyimo amesema mgonjwa huyo alifika hospitalini hapo Tarehe 13, Mei 2024 na kufanikiwa Kufanyiwa upasuaji tarehe 15 Mei 2024 na kutoa mawe hayo.

“Tumefanikiwa kuwafanyia wagonjwa wanne upasuaji mgonjwa wa kwanza ni mgonjwa aliekua na goiter ambao haitoi kichocheo, wapili alikua na mawe kwenye kibofu cha mkojo” amesema Dkt. Tito

Kwa upande wake Bw. Nard Mhunda amewashukuru Madaktari Bingwa na Bobezi katika Hospitali ya Wilaya ya Chamwino baada yakufanikisha kumtolea mawe kwenye Kibofu.

Bw. Nard, amesema mara baada yakusikia tangazo la ujio wa madaktari Bingwa na Bobezi ilimlazimu kuchukua hatua kwenda Hospitali ya Wilaya ya Chamwino kwa ajili yakuwaona wataalam hao, ambapo ndugu yake alimpeleka kwa ajili ya matibabu.

Bw. Nard amesema tatizo lake lilianza miaka kumi iliyopita, lakini hakuweza kwenda hospitalini akiamini huenda mara baada yakutumia dawa ya Mganga wa kienyeji angeweza kupona.

Bw. Nard ametumia fursa hiyo, kuiasa jamii kuepukana na mila potofu na badala yake wakipata changamoto wafike katika vituo vya kutolea huduma za afya na kukutana na wataalam wa afya pamoja na kupima afya zao mara kwa mara.

Hata hivyo, ndugu wa Bw. Nard, wameishukuru Serikali kwa ujio wa Madaktari Bingwa kusogezwa karibu na wananchi huku wakiomba iwe ni zoezi endelevu.

# RUFAA ZA WATOTO WACHANGA ZAPUNGUA KWA ASILIMIA 70% KATIKA HOSPITALI YA FRELIMO

**Na Shaban Juma**
**IRINGA**

Madaktari bingwa wa Rais Samia wamesaidia katika kupunguza rufaa ya Watoto wachanga kwa zaidi ya asilimia 70 katika hospitali ya Manispaa Iringa Frelimo baada ya uanzishwaji wa wodi ya Watoto wachanga

Hayo yamebainishwa na Mganga Mfawidhi wa Hospitali ya Manispaa ya Iringa (Frelimo) Dkt. Hassan Mtani wakati wa utoaji wa huduma za kibingwa na ubingwa bobezi kutoka kwa madaktari bingwa wa Rais Samia.

Dkt. Mtani amesema madaktari wa Rais Samia wamesaidia katika kupunguza rufaa za Watoto wachanga ambapo kwa asilimia 70 ya rufaa zilizokua zinatolewa na Hospitali hiyo ni za Watoto wachanga kwakua awali hawakuweza kulaza Watoto hao kutokana na kutokua na uwezo wa kuwahudumia juu ya changamoto wanazotokana nazo.

"uwepo wa madaktari bingwa umesaidia kuanzisha vitengo mbalimbali kama vile Wodi ya matunzo ya dharura kwa Watoto wachanga (NICU), mbali ya kuwa na vifaa lakini tulikua hatuwezi namna ya kuwasaidia Watoto ambao wamezaliwa na kupata changamoto hivyo ilikua inatulazimu kuwapa rufaa lakini kwa sasa tuna ujuzi wa kuweza kuwasaidia na kupunguza rufaa za Watoto wachanga". Amesema Dkt. Mtani.

Sambamba na hilo Dkt. Mtani amesema kuwa wamepatiwa ujuzi na kujengewa uwezo wa masuala mbalimbali ili kuweza kufanya kazi kwa weledi na kuwasaidia wananchi na ujuzi waliopatiwa kutoka kwa madaktari hao utawasaidia katika kuendelea kuboresha huduma za afya.

Hata hivyo wananchi waliojitokeza kupata huduma za madaktari bingwa wameiomba serikali kuweka utaratibu wa madaktari hao kufanya huduma hizo mara kwa mara kwani wananchi wengi wanaougua hawana gharama za kusafiri kwa ajili ya kufuata huduma za kibingwa



# MADAKTARI BINGWA WA SAMIA WAMREJESHEA FURAHA MTOTO JACKLINE



**Na Aisha Swahibu**
**SINGIDA**

Madaktari Bingwa na Bobezi wa Samia wakiwa mkoani Singida wamefanikisha upasuaji mkubwa kwa mtoto mwenye umri wa miaka mitatu aitwaye Jackline Wilson mkoani humo, na kumtolea uvimbe aliodumu nao kwa muda miaka mitatu

Akizungumza mara baada ya upasuaji huo Daktari bingwa wa Upasuaji Nassib Msuya amesema upasuaji huo ambao umefanyika katika Hospitali ya Manispaa Singida umefanyika kwa ushirikiano wa madaktari walioweka kambi katika Hospitali hiyo.

"Mtoto Jackline Wilson, amekuwa akisumbuliwa na uvimbe huu kwa muda mrefu, hali hali iliyosababisha ashindwe kushiriki kwenye majukumu ya utoto ikiwepo kucheza na wenzake" amesema Dkt. Msuya

Kwa upande wake Daktari bingwa wa ganzi na usingizi Dkt. Anna Doho amesema kuwa operesheni hiyo ilikwenda vizuri na wanatarajia mtoto huyo kupona kabisa bila matatizo yoyote ya kiafya huku akiongezea kuwa kufanikisha upasuaji huo ni ushahidi wa maende makubwa katika sekta ya afya nchini, hasa katika maeneo ya vijijini ambako huduma za upasuaji zimekuwa adimu.

Akiongea mara baada ya upasuaji huo, mzazi wa Mtoto Jaqline aitwaye Pendo Said, aliyeshindwa kuzuia hisia zake ametoa shukrani zake za dhati kwa Rais Samia na timu ya madaktari bingwa kwa jitihada zao kubwa na matibabu waliopokea.

"Tumepokea matibabu haya mkubwa kutoka kwa madaktari hawa, hatuna neno la kutosha kueleza furaha yetu. Mtoto wetu sasa ataweza kukua vizuri katika makuzi yake, amesema mama wa mtoto Bi Pendo.

Kampeni Kabambe ya Madaktari Bingwa wa Rais Samia inaendelea kuleta matumaini kwa familia nyingi nchini Tanzania, ikionyesha jinsi serikali inavyojitoa kwa dhati kuboresha maisha ya wananchi wake kupitia huduma bora za afya.

# BILA HEDHI SALAMA HAKUNA UHAI

**Na Atley Kuni**
**ARUSHA**

Mkuu wa Wilaya ya Arusha Mhe. Felician Mtahengerwa amesema ili kuwa na uhai lazima jamii izingatie suala la hedhi salama kwa watoto kike na wanawake.

Mtahengerwa amesema hayo Mei 25, 2024 jijini Arusha wakati wa hafla ya ufunguzi wa juma la Hedhi Salama nchini ambapo kilele chake kitafikia Mei 28, 2024 mwaka huu.

Akiongea katika viwanja vya Makumbusho ya Azimio la Arusha, Mhe. Mtahengerwa amesema ni jukumu la wake kwa waume kuungana kuhakikisha mwanamke anakuwa na hedhi Salama.

"Takwimu zinaonesha kwamba takriban wanawake milion 13.7 nchini wenye umri wa kati ya miaka 15 hadi 49 ambao kimsingi huwezi kupata hedhi kila siku,hivyo jamii inatakiwa kuweka mazingira wezeshi kwa mwanamke ili apate hedhi salama "Amesema mhe. Mtahengerwa.

Akizungumza kwenye hafla hiyo Mratibu wa masuala ya Hedhi salama taifa, Bi. Mariam Mashimba kutoka Wizara ya Afya amesema hedhi salama ni suala linalowezekana.

"Tunaposema hedhi salama ni hatua ya Wanawake na Wasichana kupata elimu sahihi kuhusu hedhi hivyo watumie siku za juma la hedhi salama kufika viwanja hivyo vya Makumbusho Arusha kupata elimu kutoka kwa wataalam wa afya watakaokuwepo hapo". Amesema Mariam.

Mariam amesema, suala la hedhi hutofautiana baina ya mtu na mtu na hii huweza kusababishwa na suala la lishe hivyo kila msichana au mwanamke lazima kuwa na uelewa sahihi wa hedhi na namna ya kuweza kujihudumia.

Kwa upande wake Katibu wa Jukwaa la Hedhi salama nchini Bw. Severine Alutte amesema, wanawake ni lazima wazingatie matumizi sahihi ya taulo za kike.

"Ukweli ni kwamba, taulo za kike zinaweza kuleta changamoto lakini pia matumizi yasiyo sahihi ya taulo yanaweza kusababisha madhara hivyo, kila mwanamke ni vema kuchukua tahadhari kwa kuhakikisha taulo wanazo tumia zimehakikiwa na Mamlaka ya Chakula nchini pamoja na Shirika la viwango nchini TBS" amesema Allute.

Allute amewataka wanawake na wasichana kuhakikisha wanakuwa na matumizi sahihi wanapotumia taulo hizo kwa muda uliopangwa kulingana na hali ya hedhi, huku akisisitiza kuzingatia usafi wakati wote.





# CANADA KUENDELEA KUCHANGIA MFUKO WA AFYA WA PAMOJA ILI TANZANIA KUFIKIA AFYA KWA WOTE

**Na Hassan Kimweri**
**DAR ES SALAAM**

Serikalo ya Canada imeihakikishia Tanzania kuwa itaendelea kushirikiana pamoja katika kuboresha Sekta ya Afya ili kufikia malengo ya afya kwa wote huku huduma bora za afya zikiendelea kutolewa na kupatikana kwa uhakika.

Hayo yameelezwa Mei 16, 2024 kwenye kikao kilichowakutanisha Waziri wa Afya Mhe Ummy Mwalimu na Waziri wa Maendelo ya Kimataifa wa Canada Mhe. Ahmed Hussen katika Kikao kilichofanyika katika Ofisi ndogo za Wizara ya Afya Jijini Dar Es Salaam.

"Fedha za Basket zimekuwa chanzo cha uhakika cha kugharamia huduma za afya kwenye vituo ngazi ya Zahanati hadi Hospitali za Wilaya. Zaidi ya hayo, utaratibu wa Ufadhili wa Moja kwa Moja wa Kituo cha Afya umeongeza uwajibikaji na uwazi kupitia ushirikishwaji zaidi wa jamii na ufuatiliaji wa utendaji wa matokeo ya afya ya vituo." Amesema Waziri Ummy

Pamoja na hilo, Waziri Ummy ameiomba Serikali ya Canada kusaidia na kushirikiana pamoja na Serikali ya Tanzania ili kuhakikisha utekelezaji wa Bima ya Afya kwa Wote na kusaidia uendelevu wake unafanikiwa. Hii ikijumuisha upatikanaji wa fedha pamoja na upatikanaji wa Bima kwa wananchi wote ikiwemo walio katika Sekta isiyo rasmi.

Aidha, Waziri Ummy amesema miongoni mwa mafanikio yaliyopatikana katika mashirikiano baina ya Tanzania na Canada ni pamoja na kupungua kwa kiwango cha vifo vya watoto chini ya miaka Mitano kutoka asilimia 67 mwaka 2016 hadi asilimia 43 mwaka 2022 kwa kila watoto 1,000 waliozaliwa hai.

Kwa upande wake Waziri wa Maendelo ya Kimataifa wa Canada Mhe. Ahmed Hussen ameahidi kuendeleza ushirikiano na Tanzania katika Sekta ya Afya ikiwa ni pamoja na kuendelea kuchangia katika mfuko wa Afya wa pamoja, afua za lishe, kuimarisha huduma za afya kabla ya uzazi na kuimarisha afya ya uzazi kwa wasichana na wanawake walio pembezoni.

Aidha, katika swala la Bima ya Afya kwa wote Mhe. Ahmed Hussen amesema katika nchi yao Serikali hugharamia matibabu kwa wananchi wote ambapo usimamizi wa huduma hizo hutumika kupitia Mfumo wa majimbo.

ataona wajibu wa kujitolea kwa hali na mali ili kuweza kuwafikia na kuwaibua wagonjwa wengi na kuwaweka katika matibabu ili kufikia malengo yetu ya kutokomeza ugonjwa huu". Amesema.

Waziri Ummy ameongeza kuwa mgonjwa mmoja wa kifua kikuu ambaye hajagundulika na kuwekwa katika matibabu ana uwezo wa kuambukiza watu kati ya 10 mpaka 20 kwa mwaka.

Piga picha ya mgonjwa mmoja mwenye vimelea vya ugonjwa wa kifua kikuu yupo miongoni mwa wasafiri wa mwendokasi iliyosheheni abiria au kwenye mikusanyiko na mikutano ya watu wengi kama sokoni, mialoni, kwenye kumbi za starehe kwa kutaja baadhi.

Wengi tunajua mazingira ya kwenye machimbo, mahabusu zetu, viwanja vya mipira, safari za watalii, kumbi za kuangalia sinema, makambi ya wakimbizi, mikusanyiko ya kisiasa, mabweni ya wanafunzi, makambi ya wavuvi, wazee na watoto yatima pamoja na makazi holela.

Nimejaribu kuanisha sekta tofauti tofauti, ili uweze kupata picha kuwa, tunapozungumza vita hii ni ya watu wote tuone ukubwa wa tatizo, fikiria kauli ya Waziri Ummy, halafu piga picha mtu mmoja aliyepo kwenye kanisa moja la maombezi tuone ukubwa wa tatizo.

Tuwaze juu ya biashara kubwa ya utalii ambayo inaliingizia fedha za kigeni taifa, labda uwepo wa muongoza watalii mmoja aliye na vimelea vya kifua kikuu, huku akiwa na kikundi cha watu 10 ina maana anaweza kuwaambukiza wote.

Pia tuangalie kwa jicho la tatu, sehemu za uchimbaji wa madini mbalimbali ambazo zina mikusanyiko ya watu, sio hiyo tu fikiria msanii wa muziki aliyeandaa tamasha lililo waleta watu zaidi ya 1000 kwa wakati mmoja. Pata pia picha ya abiria waliokatika madaladala na mwendokasi uliosheheni wakasafiri kila siku katika shughuli zao za kila siku.

Hapa ndipo ninapokuja na wazo kuwa vita ya kifua kikuu sio ya mtu au kundi fulani bali wadau wote kwa nguvu moja kutafuta rasilimali, kubuni afua mpya, kutoa elimu kwa kila sekta,
Mbali na miongozo iliyopo na mikakati yakukabiliana na Kifua Kikuu kwa sasa, kila nyenzo inayo onekana kufanikisha mapambano, itumike kwa maslahi mapana ya nchi.

Serikali kupitia Wizara ya Afya imefanya juhudi za kudhibiti ugonjwa huu kwa kuboresha huduma za uchunguzi na uugunduzi kufuatia kuwekeza katika tekinolojia mpya pamoja lakini pia kusambaza magari 11, mashine za Gene Xpert 50, Mashine za ECG 179 na pikipiki 179 zenye thamani ya Sh bilioni 6.8. hivi vyote ni rasilimali vitu.

Pia wajumbe wa kikao cha waratibu wa dawati linaloshughulikia kifua kikuu kwenye Wizara za kisekta waliokutana kwa siku mbili jijini Dodoma wanakuja na maazimio ambayo yanazidi yakuonesha mwanga wa kuzidi kupambana na kifua kikuu.

Baadhi ya kile kilichoadhimiwa katika mapambano ya dhidi ya ugonjwa wa kifua kikuu kuwa ni kuwa na elimu endelevu kwenye maeneo ya kazi, kuwa na taarifa za mara kwa mara zinazo elezea afua zilizo tekelezwa katika Wizara au Sekta husika.

Pia uhuishaji wa lengo la kila Wizara kuanisha wadau ambao itashirikiana nao bega kwa bega katika vita ya kutokomeza kifua kikuu nchini ni hatua muhimu sana na za kuigwa mfano.

Baada ya kuangalia ukubwa wa tatizo ni busara kila sekta kuunga mkono juhudi za Wizara ya Afya za kupambana na ugonjwa wa kifua kikuu kwa kuwekeza katika kutekeleza afua za kisekta zinazojielekeza katika vita hii.

Kupanga nikuchagua, iwapo sekta zote zitasimama kidete kuhakikisha wanakuwa mabalozi wa kukabiliana na ugonjwa huu, vita hii itafanikiwa na malengo yaliyowekwa yatatimia. Kifua kikuu kina kinazuilika na kinatibika, sote tuwajibike.





# SERIKALI, WAENDESHA BODABODA WAWEKA MIKAKATI KUTOKOMEZA AJALI

**Na Shaban Juma**
**DODOMA**

Serikali kupitia Wizara ya Afya imewapa jukumu wadau wa usafirishaji wakiwepo madereva Bodaboda na Madereva wa Mabasi kuwa vinara wa kudhibiti ajali za Barabarani ili kuokoa nguvu kazi ya Taifa.

Akizungumza katika semina na wadau wa usafirishaji Mei 11, 2024 jijini Dodoma Katibu Mkuu wa Wizara ya Afya Dkt John Jingu amesema, ajali za Barabarani zimekuwa zikichukua nguvu kazi ya taifa kwa watu walio na umri wa kati ya miaka 19 na 59.

"Mtu mmoja akipata ajali ya barabarani ambaye ndiye mzalishaji, athari zake haziishii kwa mtu binafsi bali pia jamii yake lakini pia Serikali kutumia fedha nyingi ambazo zingeweza kuelekezwa maeneo mengine kwa mustakabali na ustawi wa nchi" amesema Dkt. Jingu.

Dkt. Jingu ameongeza kuwa watu milioni 1.19 wameripotiwa kufariki Dunia kutokana na ajali za barabarani ambazo zinaongoza kwakuuwa watoto na vijana wa miaka 5 hadi 29 huku wanaofariki zaidi wakiwa ni Watembea kwa miguu, waendesha baiskeli na Bodaboda

Aidha Dkt. Jingu amesema kwa mwaka 2023 jumla ya majeruhi 163,148 walipokelewa katika vituo vyakutolea huduma za afya nchini huku mikoa ya Dar es Salaam, Morogoro, Mwanza, Dodoma na Kagera akiitaja kama mikoa inayo ongoza.

"Jumla ya majeruhi 11,434 walihudumiwa kwenye Hospitali 16 za Rufaa za Mikoa 16 nchini kwa kipindi cha mwezi Juni 2023 hadi Machi 2024 majeruhi wa Bodaboda wakiwa asilimia 61 ya majeruhi wote" amefafanua Dkt. Jingu.

Awali, Mganga Mkuu wa Serikali Prof. Tumaini Nagu, akimkaribisha Katibu Mkuu kufungua semina hiyo, amesema shabaha yakuwaita wadau wa usafiri nikuweka Mikakati ya pamoja kukabiliana na ajali Barabarani.

Akitoa mada kwenye Semina hiyo, Kamishna Msaidizi Polisi Mkuu wa Dawati la Elimu kwa umma Makao Makuu, Michael Deleli, ameendelea kuwahimiza wapanda pikipiki kuvaa kofia Ngumu.

"Kichwa hakina mbadala wake, kikiumia huwezi kusema utaweza kubadilisha, rai yangu hakikisha wewe dereva na abiria wako mnajihami kwakuvaa Kofia Ngumu kujikinga na Ajali lakini pia kuacha ulevi wakati wa kazi" amesema ACP Michael Deleli

# DKT. JINGU AWAFUNDA WASIMAMIZI WA MIRADI WIZARA YA AFYA

**Na Abdulwaheed Madenge**
**DAR ES SALAAM**

Katibu Mkuu wa Wizara ya Afya Dkt. John Jingu amewapa somo Wasimamizi wa Miradi Wizara ya Afya juu ya umuhimu wa kuhakikisha Miradi ya Maende inaimarisha Maisha na uasalama wa Wananchi kwa kukidhi mahitaji kijamii, na kuleta matokeo chanya yenye manufaa na tija kwa jamii na sio kuiangamiza.

Dkt. John Jingu, amesema hayo Mei 23, 2024 Jijini Dar es Salaam wakati akifunga kikao kazi cha Kuboresha utendaji kazi kilichokutanisha Wakurugenzi, Wakurugenzi wasaidizi, Mameneja, Wakuu wa progarmu, waratibu wa Miradi na baadhi ya Maafisa wanaosimamia utelezeji wa Miradi hiyo kutoka Wizara ya Afya.

"Kwenye utekelezaji wa miradi hasa kwenye sekta hii ya Afya ambayo inamgusa mwananchi moja kwa moja ukifanya makosa tu au ukifanya ka uzembe inawezekana watu wakapaoteza maisha ama wakapata ulemavu wa maisha hivyo Makosa kwetu hayakubaliki sababu Madhara ya Makosa kwenye sekta yetu ni hatari kwa jamii" amesema Dkt. Jingu.

Amesema kwa kuliona hilo Wizara ya Afya imeamua kufanya Kikao kazi hiki ili kuboresha utendaji kazi kwa kuwafundisha namna bora ya utekelezaji wa Miradi na kuipusha jamii na Makosa yanayo zuilika.

"Kama watumishi wa umma ni Muhimu kukumbushana, kufundishana na kuelekeza umuhimu na wajibu wetu ni upi, Nini kinatarajiwa kutoka kwetu baada ya hapo ukikosea kwa makosa ambayo yanazuilika hapo unatakuwa umefanya kusudi nasi hatutalifumbia macho hilo" aliongeza Dkt. Jingu

Dkt. Jingu pia amatumia fursa hiyo kuwasihi watumishi wa umma na wale wasio wa umma kuhusu suala la Maadili.

"Tuzingatie Maadili ya kazi zetu, Maadili ya kazi zetu kila mtu kwa eneo lake na maadili ya Utumishi wa Umma Kwa ujumla wake, hata ukiwa Mtumishi wa ajira za mkataba wa siku moja ni lazima ufuate Maadili ya Utumishi wa Umma kwani Maadili haya yanatuhusu wote"

Nae Afisa wa Serikali Haika Msuya aliyetoa mada katika kikao hicho, amewasihi washiriki hao wa kikao kazi hicho kuendelea kufanya kazi kwa Bidii ili kukidhi mahitaji ya wanachi walio wengi kwa kuzingatia kanuni za utumishi wa Umma



TDA TANZANIA DIGITAL AWARDS

Innovation Week Tanzania 2024

IMPLEMENTED BY: SERENGETI BYTES

Best Government Ministry on Digital

# WINNER

UHURU NA UMOJA

**Ministry of Health**




**Jarida hili limeandaliwa na Kitengo cha Mawasiliano Serikalini**
**WIZARA YA AFYA, TANZANIA, TOLEO LA MWEZI MEI, 2024**